

Public education  
Discover a world of opportunities

# KUANDIKA NA HERUFI: KUSOMEA NYUMBANI

## KUANDIKA NA KUSEMA HERUFI NI MHIMU!

Kuzungumza na kusikiliza ndiyo misingi wa maandishi, herufi na kusoma. Katika Miaka 1 na 2 watoto wako huwa wazoefu zaidi wa maneno na herufi. Wakati kujiamini kwao kunaongezeka, wataanza kujumuisha kuandika katika shughuli zao za kila siku.

### Ni naweza kufanya nini?

- Kuchunguza maneno na vitabu pamoja. Kusoma mara kwa mara pamoja na kuhimiza watoto wako kusoma na wewe kila siku.
- Kuhimiza watoto wako kufanya mazoezi ya uandishi mara kwa mara.

**Zima televisheni. Ni rahisi mtoto wako kuweza kutulia kama hakuna vitu vya kumhagaisha.**

Ikiwa watoto wako huzungumza lugha nyingine au lahaja, wanahitaji muda wa kusikia sauti ya lugha ya Kiingereza. Inaweza kuchukua hadi miaka miwili au zaidi kwa wao kusikia na kusema sauti hizi zote.

- Kutafuta maneno nyumbani, na wakati uko nje na sehemu zingine, wakati unatembea na ukiwa unasafirri kama vile ishara za kwenye maduka
- Kuanzisha bao wa ujumbe wa nyumbani na kuandika ujumbe kwa watoto wako. Kuwatia moyo kuacha ujumbe kwa ajiri yako na ndugu wengine wa familia
- Kuandika ujumbe mbalimbali pamoja kila siku, kama vile utaratibu wa chakula cha mchana cha watoto wako na maelezo kwa wanafamilia wengine



Department of  
Education

**Utapata zaidi  
Kijitabu cha ukweli cha kusomea nyumbani  
Kwenye elimu hapa: [education.wa.edu.au](http://education.wa.edu.au).**

# KUANDIKA NA HERUFI: KUSOMEA NYUMBANI

**Mtoto mlemau kwa kawaida anafaidika na kufurahia kutokana na mwingiliano wa karibu na kusisimua unaotolewa wanapokuwa wakisoma hadithi wanazozipenda au nyimbo zinazoimbwa za kitalu. Kama mtoto wako ana ulemavu, shule zao zinasaidia wao kwa kushiriki katika shughuli katika ngazi zinazofaa kwa uwezo wao. zungumza na mwalimu wa mtoto wako kuhusu zana sahihi, vifaa na mawazo ya kusaidia wewe na mtoto wako.**

- Kukaa chini na watoto wako na kufanya orodha ya maneno wanayoyapenda. Soma hizi orodha pamoja nawao mara kwa mara. Onyesha orodha katika maeneo wazi ndivyo iwe rahisi kwa watoto wako kuyaona.
- Kuuliza watoto wako kujaribisha katika kusema maneno ya herufi kabla ya kuwapa majibu sahihi.

- Kufanya matumizi mazuri ya barua usizozihitaji! Uliza watoto wako ku:
  - zungushia maneno yenye baadhi ya herufi kama vile *na* na baadhi ya sauti *kama* *vile*
  - kusisitiza maneno yote mawili ya herufi, herufi tatu za meneno na kadhalika
  - hesabu ni mara ngapi wanaweza kupata neno fulani kama *vile* – hii inasaidia kutambua maneno ya kawaida.

**Ni muhimu kukumbuka kwamba watoto wanaendelea kwa viwango tofauti. Kuwa na subira, furahia na kuunga mkono, na kuwa na uhakika wa kuwasifia ili waendelee hata kama hawajapata majibu sahihi.**

